**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI MHE. ENG. EVARIST NDIKILO WAKATI WA UFUNGUZI WA WARSHA YA KONGANO LA VIWANDA, TAREHE 27 JANUARI, 2021 KWENYE UKUMBI WA MKUTANO WA OFISI YA MKUU WA MKOA WA PWANI - KIBAHA**

- ***Katibu Tawala Mkoa,***
- ***Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa SIDO,***
- ***Meneja wa Sido Mkoa wa Pwani,***
- ***Makatibu Tawala Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo Sekretarieti ya Mkoa,***
- ***Wakurugenzi wa Halmashauri,***
- ***Mwakilishi toka CBE,***
- ***Mwakilishi wa Chemba ya wafanyabiashara, Kilimo, Viwanda (TCCIA),***
- ***Jumuiya ya Wafanyabiashara Pwani,***
- ***Mwakilishi kutoka TARI,***
- ***Kiongozi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi,***
- ***Wataalam ngazi ya Mkoa na Halmashauri,***
- ***Waandishi wa habari,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

***Ndugu Washiriki,***

Awali ya yote, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kutuwezesha kukutana hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Nichukue nafasi hii kuwashukuru wote kwa kuhudhuria semina hii ambayo

ni muhimu sana kwa Mkoa wetu hasa wakati huu ambao tupo kwenye harakati za kufanya nchi yetu kuwa ya viwanda chini ya uongozi thabiti wa Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kushiriki kwenu kunatoa fursa ya kujifunza na kuelewa vizuri hii dhana ya Kongano la Viwanda ambalo tunaamini italeta tija katika kuanzisha na kuendeleza viwanda katika Mkoa wetu.

***Ndugu Washiriki,***

Pia niwashukuru wenzetu wa Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo, (SIDO) kuleta semina hii ambayo kwa hakika tukiipokea na kuifanyia kazi itatuwezesha kuweka mikakati mizuri ya uwekezaji endelevu wa Viwanda katika Mkoani wetu. Viongozi wa SIDO mlioko hapa naomba mtufikishie salamu zetu kwa Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, mwambie Mkoa wa Pwani tunashukuru na tunaahidi kuendelea kutoa ushirikiano na SIDO. Ulivyonialika jana nikasema jambo hili ni muhimu na kubwa lazima nishiriki.

***Ndugu Washiriki,***

Lengo la Warsha hii ni kupata uelewa wa pamoja kuhusu dhana ya Kongano na jinsi gani tunaweza kuitumia katika kuanzisha na kuendeleza Viwanda katika Mkoa wetu.

Kongano ni mkusanyiko wa viwanda vilivyo karibu karibu vinavyofanya shughuli zinazofanana au kushabiana zikisaidiwa na watoa huduma mbalimbali.

Dhana ya uendelezaji wa Kongano ni njia ya kutambua faida za kiushindani kwa kuwezesha na kuimarisha uunganishwaji na ushirikiano baina ya wadau mbalimbali waliopo kwenye mnyororo wa thamani.

Muunganisho na ushirikiano huo unawezesha wajasiriamali kupata fursa na faida nyingi kama vile ***kupata teknolojia, kuongeza ujuzi, kupata taarifa, masoko na huduma wezeshi kama vile TBS, MDA***.

***Ndugu Washiriki,***

Nimetaarifiwa hadi sasa takriban Kongano 59 zimetambuliwa nchini na zinahudumiwa na SIDO kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo. Kongano hizo zinapatikana Mikoa ya Mwanza (Ngozi), Kagera (Bidhaa za chuma), Singida (Kusafisha mafuta ya Alizeti), Kilimanjaro (Maziwa), Mbeya (Mpunga) na Shinyanga (Katani). Bahati mbaya kwa Mkoa wetu wa Pwani utekelezaji wa dhana ya Kongano bado haujaanza. Kwa kuwa Mkoa wetu unazo fursa nyingi za Uwekezaji wa Viwanda, warsha hii ya Kongano imekuja wakati muafaka.

***Ndugu Washiriki,***

Nafasi ya Mikoa na Wilaya katika ujenzi wa Viwanda kwa kufuata Mwongozo wa Taifa wa Uanzishwaji wa Viwanda kila Mkoa ni pamoja na kufanya yafuatayo:-

i. Kuwezesha ujenzi na uendelezaji wa kongano *(cluster)* zitakazotumika hasa na sekta ya viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati. Kongano hizi pia ziwe na maeneo ya kuhifadhi malighafi na bidhaa zitakazozalishwa pamoja na sehemu za kufanyia mauzo ya bidhaa husika ili kuondoa msongamano usio wa lazima wa kuuza bidhaa hizo katikati ya miji. Kongano hizi pia zitarahisisha utolewaji wa huduma za miundombinu, uzalishaji bora na kwa wingi, huduma za kuendeleza biashara zinazotolewa na taasisi za umma na binafsi na upatikanaji wa mitaji kutoka katika vyombo vya fedha.

***ii.*** Kutengeneza Wajihi za kiuchumi na Mwongozo wa Uwekezaji *(Investment Guide)* wa Mikoa na Wilaya ambazo zitatoa kwa ufasaha taarifa na fursa za kiuchumi na uwekezaji ambazo pia ni fursa za uwekezaji katika viwanda kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

***iii.*** Kuanzisha madawati na Kamati za Viwanda na Uwekezaji ngazi ya Mkoa na Halmashauri ambapo masuala ya viwanda yanashughulikiwa kwa ukaribu

iv. Viongozi wa Mkoa na Wilaya tumekuwa tukitembelea na kufuatilia Miradi ya Sekta binafsi iliyoanzishwa ili kujua changamoto wanazokumbana nazo na kuzitatua.

v. Tumeanzisha na Kufanya Maonesho ya Viwanda kwa Miaka miwili Mfululizo lengo likiwa kutafuta masoko na kuwahudumia kwa karibu wawekezaji wetu.

vi. Tumeendelea kufanya Vikao vya Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya ambayo hukutana kujadili namna ya Kuboresha Mazingira ya Kufanyia biashara na uwekezaji.

***Ndugu Washiriki,***

Mkoa wetu tulijipambanua tangu mwaka 2015 Kuwa Ukanda wa Viwanda. Mikoa jirani inatamani kuja kujifunza kwetu mapinduzi haya ya Viwanda ambayo sisi tunayaongoza katika Nchi, Mwaka 2015 tulikuwa na viwanda 395, Mwaka 2020 tumefikia viwanda 1,236 **vikubwa 68, vya kati 112, vidogo 168 na Vidogo sana 888.** Nilishawaambia mara kadhaa siri ya mafanikio ya Mapinduzi ya Viwanda kwenye Mkoa wetu ni pamoja na;

i. Kuzungumza lugha moja sisi Viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi Mkoani,

ii. Kuondoa urasimu katika kutoa huduma kwa wawekezaji, viongozi na maafisa wa njoo kesho na kuzungusha wawekezaji hatuwavumilii kabisa.

Warsha hii ya Kongano imekuja wakati muafaka na ni matumaini yangu Mkoa wa Pwani unakwenda kusomeka katika Mikoa iliyofanikiwa kuanzisha Kongano. Niwaombe Viongozi wenzangu tudhamirie kukamilisha uanzishwaji wa Kongano hizi. Tuache Uvivu na kukwepa majukumu kuanzia Mkoani hapa (Regional Secretariat) (RAS, DCs, DED AASE, Afisa Biashara Mkoa na Walezi wote wa Halmashauri) tutekeleze majukumu tutakayopangiana hapa.

***Ndugu Washiriki,***

Nimatumaini yangu kuwa baada ya warsha hii mambo yafuatayo yataaza mara moja kutekelezwa;

I. Kuandaa mpango wa ujenzi wa Viwanda katika maeneo yaliyotengwa kulingana na aina za viwanda.

II. Kuchagua mazao ya kimkakati kwa ajili ya malighafi za Viwanda (mfano: Nazi kwa Mafia, Mhogo kwa Wilaya za Mkuranga, Kibiti, na Kibaha. Matunda kwa Wilaya ya Bagamoyo).

III. Kuandaa mpango kazi wa utekelezaji wa dhana ya Kongano na kuingiza kwenye mipango ya maendeleo ya Halmashauri.

Mkoa utaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa dhana hii katika Halmashauri zote ili tuweze kufikia azma ya Serikali ya kuanzisha Viwanda. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumefanikiwa kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano awamu ya Pili (FYDP II; 2016/17 – 2020/21) unaozitaka Halmashauri kuendeleza Kongano za Biashara Ndogo na Kati zinazolenga kuimarisha upatikanaji wa pamoja wa malighafi za Viwanda vya ndani.

***Ndugu Washiriki,***

Mwisho niwatakie majadiliano mazuri ili muweze kutoka na uelewa wa pamoja utakaowezesha utekelezaji wa dhana ya Kongano la Viwanda. Pia niwatakie kila la kheri katika kuandaa mipango ya utekelezaji wa dhana ya kongano katika maeneo yenu.

***Ndugu Washiriki,***

Baada ya kusema hayo, sasa natamka kwamba warsha ya siku moja kuhusu uanzishwaji wa Kongano Mkoa wa Pwani imefunguliwa rasmi.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**